# Nafasi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi nchini Kenya: Majukumu na Changamoto

*Jim Ontieri*


## Ikisiri

Kiswahili ndiyo lugha ya taifa nchini Kenya na kwa kiasi kikubwa inaeleweka na kutumiwa na Wakenya wengi kwa ajili ya mawasiliano ya kila siku. Ingawa kwa miaka mingi, lugha hii imetajwa kama lugha rasmi, hususani katika mawasiliano bungeni, katiba ya zamani haikuitambua kama lugha rasmi. Katiba mpya inakitambua Kiswahili kama lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Hali hii inamaanisha kwamba, lugha hii imepewa majukumu mapya ya kimatumizi nchini Kenya. Kinyume na wakati ambapo lugha ya Kiswahili imekuwa ikipuuzwa na hata kuchukuliwa kama lugha ya wasio na elimu ya kisasa, lugha hii sasa imepewa hadhi katika jamii ya Wakenya wa matabaka mbalimbali. Ni wazi kuwa hali hii mpya itachangia pakubwa katika kutimizwa kwa ndoto ya wasomi wa Kiswahili na hata viongozi wa kisiasa barani Afrika ambao wamekuwa wakipendekeza kuwa Kiswahili kiwe lugha inayotumiwa katika shughuli rasmi kote barani Afrika. Kwa sasa Kiswahili ndiyo lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na imependekezwa kama lugha mojawapo ya Muungano wa Afrika (Momanyi, 2009). Kenya ikiwa nchi mojawapo iliyo na ukwasi mkubwa wa kimatumizi wa Kiswahili barani Afrika, ina nafasi ya kipekee ya kueneza matumizi ya lugha hii nchini na barani. Hili ni jambo ambalo kwa kweli limepewa msukumo mkubwa kutokana na Kiswahili kupewa hadhi ya lugha rasmi nchini Kenya. Suala kuu litakalowekwa wazi katika makala haya ni majukumu ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali miongoni mwa wananchi wa Kenya. Aidha, changamoto anuwai zinazotarajiwa kuikumba lugha hii katika utekelezaji wa majukumu husika, zitajadiliwa.


## 1.0 Utangulizi

Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii. Kiswahili ni lugha iliyo na asili yake barani Afrika. Hii ni moja ya lugha za Kibantu ambazo huzungumzwa kusini mwa Ikweta barani Afrika. Kiswahili kama lugha ya Kiafrika ina majukumu anuwai katika nchi mbalimbali, hususani nchini Kenya. Hali hii inatokana na hatua ya lugha hii kupewa hadhi mpya kama lugha rasmi kwa mujibu wa katiba mpya ya mwaka 2010. Ni kutokana na mabadiliko haya ambapo makala yanachunguza majukumu ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini; changamoto zinazotarajiwa kuikumba lugha hii katika utekelezaji wa majukumu yake huku mapendekezo yakitolewa kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto husika. Ikumbukwe kwamba lugha hii itaendelea kutekeleza majukumu yake ya awali kama lugha ya taifa ambayo inawaunganisha Wakenya wote. Aidha, hii ndiyo lugha iliyo na matumizi mapana katika jamii ya Wakenya. Kwa mujibu wa Kimemia (2001:12), Kiswahili ndiyo lugha ya matumizi mapana kwa Wakenya wengi ambao huitumia katika shughuli za kijamii na zile za kiuchumi. Hali hii mpya inaifanya Kenya kujiunga na mataifa mengine ulimwenguni (isipokuwa Afrika na Osheania ya weusi) ambayo hutumia lugha ya taifa kama lugha rasmi. Mataifa mengine ya Afrika na yale ya Osheania ya weusi, hutumia lugha tofauti kutekeleza majukumu ya kitaifa na yale

rasmi. Ni nadra sana kupata lugha moja ikichukua nafasi ya lugha ya taifa na ile rasmi katika nchi zilizoko katika maeneo haya yaliyotajwa.

## 2.0 Majukumu ya Kiswahili kama Lugha Rasmi

Lugha rasmi huwa na majukumu mbalimbali katika jamii. Hii ndiyo lugha ambayo hutumiwa kama nyenzo ya kufundishia shuleni na vyuoni. Mbali na lugha hii kufundishwa kama somo, inatarajiwa kwamba itatumiwa kufundishia masomo mengine katika mfumo wa elimu. Jambo hili linabainika tunaporejelea matumizi ya Kiingereza (lugha rasmi) nchini Kenya. Wakirejelea pendekezo mojawapo la Kamati ya Elimu ya Ominde (1964), Bunyi (1999) na Mbaabu (1996), wanaeleza kwamba haikuipa lugha ya Kiswahili nafasi ya lugha ya kufundishia ingawa ilikuwa na utajiri wa maandishi na ilitumiwa na Wakenya wengi katika mawasiliano. Wakati ambapo Kiingereza hutumiwa kufundishia masomo mengine kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu, Kiswahili kwa upande mwingine hufundishwa kama somo. Tukichukua mfano wa Quebec ambapo mageuzi katika katiba yalipelekea Kifaransa kutambuliwa kama lugha rasmi; lugha hii ilianza kutumiwa katika kufundishia masomo mengine kuanzia shule za chekechea hadi zile za upili (John, 1998; Patel, 2000). Kutokana na hadhi mpya, Kiswahili kinatarajiwa kuanza kutumiwa kufundishia masomo mengine katika viwango mbalimbali vya elimu nchini. Hili ni jukumu ambalo linahitaji maandalizi yenye msingi imara. Ni muhimu kutaja hapa kwamba, maandalizi hayo yatahusu utayarishaji wa mtalaa mpya wa elimu katika viwango mbalimbali. Aidha, vitabu vitakavyohitajika ili kufundishia masomo katika viwango anuwai vya elimu sharti viandikwe kwa Kiswahili. Mafunzo kwa walimu vyuoni yanatarajiwa kufanywa kwa Kiswahili kama njia ya kuwaandaa wahusika kufundisha katika taasisi za elimu nchini. Maafisa wa elimu katika ngazi tofautitofauti watahitajika kujifunza Kiswahili ili kujitayarisha kwa jukumu la kuelekeza mipango ya elimu katika maeneo yao. Hali hii inatarajiwa kudhihirika katika taasisi za elimu ya juu kama vile vyuo vikuu ambavyo vitatakiwa kuweka mikakati imara ya kuziwezesha kuimarisha mawasiliano kwa Kiswahili miongoni mwa wataalamu wa masomo mbalimbali. Hii inamaanisha kuwa lugha ya Kiswahili itastawishwa sambamba na Kiingereza (lugha rasmi tangu Kenya ilipojinyakulia uhuru) ili kukidhi mahitaji ya kufundishia masomo mbalimbali.

Kiswahili ndiyo lugha mojawapo ambayo itatumiwa katika mfumo wa sheria nchini. Mnamo mwaka 1974, rais wa kwanza wa Kenya, Hayati Mzee Jomo Kenyatta, alitangaza kuwa Kiswahili kingekuwa lugha rasmi na hata kutumiwa katika mijadala bungeni. Wakati huo wanasiasa wengi waliipinga hatua hiyo huku mwanasheria mkuu wa kipindi hicho akisisitiza kuwa ilikuwa vigumu kutafsiri vifungu vya sheria kwa Kiswahili. Kutokana na kutambuliwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi nchini katika katiba mpya, inatarajiwa kwamba lugha hii itatumiwa sambamba na Kiingereza katika kitengo cha sheria. Tafsiri ya sheria kwa Kiswahili ni kati ya michakato ambayo inastahili kuendelezwa ili kutimiza lengo la kuimarisha matumizi ya lugha hii katika

kitengo cha sheria. Matumizi kama haya yanadhihirika katika nchi mbalimbali ulimwenguni ambapo lugha rasmi ndizo hutumiwa katika mfumo wa sheria. Kwa mfano, nchini India, masuala ya kisheria huendeshwa kwa Kiingereza, lugha rasmi ya nchi hiyo (Kachru, 1986:7). Aidha, hali kama hii ilijitokeza kule Quebec ambapo baada ya Kifaransa kutambuliwa kama lugha rasmi sambamba na Kiingereza, masuala ya mahakama yalianza kuendeshwa kwa lugha hizo mbili. Ilisisitizwa kwamba wananchi walikuwa na uhuru wa kutumia lugha mojawapo kati ya hizo mbili mahakamani na hata kuomba tafsiri ya hukumu kwa lugha hizo (Richard, 1984). Ukalimani unaohimizwa hasa mahakamani utapungua ikiwa lugha hii ambayo inatumiwa na Wakenya wengi itachukua nafasi yake kama lugha rasmi ya shughuli za mahakama. Mabadiliko kuhusu lugha rasmi kwa mujibu wa katiba mpya, yatapelekea rekodi za mahakama zinazoandikwa kwa Kiingereza, kuandikwa pia kwa Kiswahili.

Biashara kati ya nchi moja na nyingine huendeshwa kwa lugha inayoeleweka kwa pande mbili zinazohusika. Lugha hiyo aghalabu huwa lugha rasmi katika nchi zinazohusika katika biashara. Tunapotazama hali ilivyo nchini Kenya, Kiingereza ndiyo lugha inayotumiwa katika biashara na nchi za nje, hususani zile zinazotumia lugha hii. Matumizi haya yamekuwa yakiendelea kwa miaka mingi na upeo uliofikiwa hauna kipimo. Kiswahili kinastahili kutumiwa katika kuendeleza biashara ya kimataifa sambamba na Kiingereza. Ni wazi kuwa biashara ni muhimu katika uimarikaji wa uchumi wa nchi yoyote. Hivyo basi, matumizi ya Kiswahili katika biashara ya kimataifa, yanatarajiwa kupewa kipaumbele kama njia ya kukuza lugha hii mpya rasmi. Hali hii mpya inaweza kuendeleza biashara, hususani kati ya nchi ambazo hutumia Kiswahili kwa mawasiliano.

Lugha rasmi ndiyo inayotumiwa na serikali katika kuendeshea shughuli zake. Hii ni nafasi ambayo imechukuliwa na Kiingereza nchini Kenya kwa muda mrefu. Katika hali hii mpya, Kiswahili ni kati ya lugha mbili ambazo zitakuwa zikitumika katika nyanja mbalimbali za serikali. Miongoni mwa masuala ambayo yatahitaji kushughulikiwa kwa Kiswahili ni pamoja na: mijadala bungeni, mawasiliano kati ya viongozi wa taifa na wananchi, mawasiliano katika ofisi za umma, na katika mikutano ya kisiasa. Katika juhudi za kutekeleza majukumu hayo, lugha ya Kiswahili itahitaji kuratibiwa upya kupitia kauli za kisera kutoka kwa viongozi wa kisiasa nchini. Mawasiliano ya kisiasa mashinani yamekuwa yakitumia Kiswahili na lugha za kienyeji kama nyenzo muhimu huku mipango ya kisiasa ya serikali kuu ikiwa inaendeshwa kupitia Kiingereza. Mtandao wa kiutawala nchini utahitaji kufanyiwa mabadiliko ili kuiwezesha lugha hii mpya rasmi kutumika sambamba na Kiingereza katika kukidhi mahitaji ya mawasiliano nchini.

Sayansi na teknolojia huenezwa kwa lugha rasmi. Maendeleo katika uwanja huu ni muhimu kwa nchi yoyote ulimwenguni. Maarifa katika sekta hiyo ni kichocheo kikuu cha ustawi wa jamii, hususani kiuchumi. Ili lugha ya Kiswahili iweze kutumika katika

shughuli za kisayansi na kiteknolojia, istilahi za kurejelea masuala mbalimbali husika zitahitaji kubuniwa na kusanifishwa. Ni kupitia juhudi hizi ambapo lugha hii itakuwa na uwezo wa kutumika katika sekta hii huku ikikumbukwa kuwa dhana husika ni ngeni na zimekuwa zikirejelewa kwa Kiingereza kwa miaka mingi. Teknolojia ya mawasiliano na tovuti kwenye mtandao, hutumia lugha ya Kiingereza kwa kiasi kikubwa. Hapa ndipo lugha ya Kiswahili itahitaji kuimarishwa ili ichukue nafasi muhimu katika mawasiliano ya aina hiyo.

Lugha rasmi huenezwa kupitia nyenzo mbalimbali, hususani vyombo vya habari kama redio, runinga na magazeti. Hali ya Kiswahili nchini Kenya imekuwa ikiimarika kutokana na matumizi ya redio na televisheni. Vituo vingi vya habari hutumia Kiswahili na Kiingereza katika utangazaji. Inatarajiwa kwamba lugha rasmi itapewa nafasi maalumu katika vituo vya kitaifa vya utangazaji wa habari. Aidha, hii ndiyo lugha ambayo inastahili kutumiwa katika magazeti ambayo husambazwa kote nchini. Miongoni mwa magazeti yanayochapishwa na kusambazwa nchini Kenya, ni gazeti moja pekee *(Taifa Leo)* ambalo huandikwa kwa Kiswahili. Kwa kuwa lugha hii inaeleweka na hata kutumiwa na Wakenya wengi, basi juhudi zielekezwe katika uchapishaji na usambazaji wa magazeti yaliyoandikwa kwa Kiswahili.

## 3.0 Changamoto kwa Kiswahili kama Lugha Rasmi

Kiingereza imekuwa ndiyo lugha rasmi tangu Kenya ilipojinyakulia uhuru. Hali hii imeiwezesha kukita mizizi kimatumizi katika nyanja mbalimbali. Kunatarajiwa kuzuka changamoto kwa Kiswahili kupenya na kutumiwa kama lugha rasmi katika nyanja tofauti ambapo lugha ya Kiingereza imezoeleka. Hili ni tatizo ambalo limewahi kuzikumba nchi mbalimbali ulimwenguni ambazo katika kipindi fulani zimeanza kutumia lugha mpya kama lugha rasmi ilhali pamekuwepo lugha nyingine rasmi ambayo imezoeleka. Kwa mfano, nchini Afrika Kusini, katiba mpya ilitambua lugha nyingine tisa (isiNdebele, isiXhosa, isiZulu, Sepedi, Sesotho, Setswana, SiSwati, Tshivenda na Xitsonga), mbali na zile za awali (Kiingereza na Kiafrikana). Hata hivyo, sera hii imekumbwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wake. Kiingereza na Kiafrikana ndizo lugha ambazo zinaendelea kutumiwa katika elimu, masuala ya kiuchumi, na taasisi za umma. Wananchi ambao hawatumii lugha hizo wamejikuta wametengwa katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Changamoto kama hii inaweza kuukumba utekelezaji wa azimio la kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi.

Suala la istilahi, hususani za sayansi na teknolojia ni changamoto nyingine kwa Kiswahili katika hadhi yake mpya. Ingawa lugha hii inatumiwa na kueleweka miongoni mwa Wakenya wengi, juhudi hazijafanywa, za kubuni na kusambaza istilahi katika nyanja hizo mbili. Hali hii itakwaza matumizi ya Kiswahili katika nyanja husika. Tukichukua mfano wa ujumbe unaotokea kwenye vijikaratasi

vinavyowekwa kwenye makasha ya dawa wakati wa kufungashwa, ni muhimu ujumbe huo uandikwe kwa lugha rasmi za nchi ambamo dawa hizo zitauzwa. Hivyo basi, lugha ya Kiswahili itatarajiwa kujitosheleza kimsamiati kiasi cha kuweza kutumiwa katika matibabu ili hadhi yake iimarike.

Mielekeo ya baadhi ya Wakenya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili itakwaza kukubalika kwake kama lugha rasmi. Kwa mujibu wa Fasold (1984: 148), mielekeo kuhusu lugha yaweza kuilenga lugha husika, wasemaji wake, masuala ya uimarishwaji wa lugha hiyo au juhudi za upangaji wa lugha husika. Wasomi wengi katika nyanja mbalimbali isipokuwa wanataaluma wa Kiswahili, wamezoea kutumia Kiingereza katika shughuli zao za kikazi. Hii ni hali ambayo imekuwa ikiendelea tangu Kenya ilipojinyakulia uhuru. Aidha, ni wasomi wachache miongoni mwa hao walio na mitazamo hasi dhidi ya Kiswahili, wanaoweza kuwasilisha mawazo yao kwa Kiswahili sanifu. Kikundi hiki kinatarajiwa kuendelea kutumia Kiingereza katika mawasiliano na kupuuza Kiswahili hata baada ya lugha hii kupewa hadhi mpya. Akieleza kuhusu hali ilivyokuwa nchini India, Naya (1969:98), anasema kuwa hata baada ya Kihindi kutambuliwa kama lugha rasmi sambamba na Kiingereza, wasomi wengi walipendelea Kiingereza wakati wa kutoa huduma katika ofisi za serikali. Naye Tully (1997:161-2), anaeleza kuwa nchini India, Kiingereza ndiyo lugha inayowaunganisha watu wenye uwezo katika jamii. Hali hii imepelekea kutengwa na kupuuzwa kwa umma. Hivyo basi, itakuwa vigumu kwa Kiswahili kupenya katika maeneo mbalimbali ya kitaaluma ambayo yanaongozwa na wasomi ambao wana mitazamo hasi kuhusu lugha husika.

Pana ukosefu wa miundombinu thabiti ya kuendeleza Kiswahili nchini Kenya. Ingawa kuna vyama mbalimbali vya kitaaluma vinavyoshughulikia masuala anuwai ya Kiswahili, serikali haijabuni chombo maalumu kilicho na uwezo wa kusimamia shughuli husika. Hali hii inatarajiwa kutatiza mikakati ya vyama hivyo katika kuiwekea lugha ya Kiswahili msingi imara huku ikilenga kupenya katika nyanja mbalimbali nchini. Ikiwa juhudi za wadau katika shughuli za uendelezaji wa Kiswahili zitaendeshwa bila kuratibiwa upya, basi pana uwezekano wa kuzuka kwa mitazamo inayokinzana kuhusu matumizi ya lugha hiyo. Kwa mfano, vyama husika vinaweza kubuni istilahi tofauti kurejelea dhana moja na hivyo kuwakanganya watumiaji wa lugha ya Kiswahili nchini.

## 4.0 Mapendekezo na Hitimisho

Wanataaluma wa Kiswahili nchini wanapaswa kuunda baraza maalumu la kushirikisha shughuli za kuendeleza matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi. Baraza hili lijihusishe na usawazishaji wa istilahi zitakazobuniwa kurejelea mambo mbalimbali katika nyanja zilizo na upungufu wa istilahi za Kiswahili. Juhudi za

baraza la aina hii zitapelekea kuwepo kwa vigezo maalumu na vinavyokubalika vya kutathmini istilahi zilizobuniwa na kuamua kuhusu ufaafu wake na kinyume chake.

Serikali inapaswa kutenga rasilimali kwa ajili ya kueneza matumizi ya Kiswahili nchini. Kwa mujibu wa Shitemi (2011), serikali inatakiwa kutambua umuhimu mkubwa wa lugha hii nchini na hivyo kutenga fedha zitakazotumiwa kuisambaza katika maeneo yote nchini, hasa baada ya kupewa hadhi mpya kama lugha rasmi. Kupitia ufadhili wa serikali, wanataaluma wa Kiswahili watakuwa katika nafasi nzuri ya kuendeleza mipango ya kueneza lugha hii kimatumizi katika sekta mbalimbali. Shughuli za utafiti zitaendeshwa na mikakati ya kubuni istilahi faafu kuimarishwa kutokana na fedha zitakazotolewa na serikali. Aidha, uchapishaji wa vitabu na majarida, utawezekana, kwa lengo la kusambaza istilahi mpya kote nchini.

Vyombo vya habari ni muhimu katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi. Ingawa lugha ya Kiswahili imepewa nafasi katika vyombo vya habari nchini, utaratibu mpya wapaswa kuanzishwa ili kuviwezesha vyombo husika kuchangia katika uenezaji wa lugha sanifu katika sekta mbalimbali. Hili litawezekana kupitia ushirikiano kati ya vyombo husika na wataalamu wa Kiswahili katika kuimarisha mikakati ya kusahilisha matumizi ya lugha hii kwa manufaa ya wananchi wote. Vipindi maalumu vinastahili kuanzishwa katika idhaa mbalimbali za utangazaji, ambavyo vitaweka wazi sera mpya ya lugha kwa mujibu wa katiba mpya huku wananchi wakielekezwa kuhusu umuhimu wa Kiswahili kama lugha rasmi. Aidha, uandishi na uchapishaji wa magazeti na majarida ya Kiswahili upewe msukumo kwa lengo la kuistawisha lugha hii.

Viongozi wa kisiasa watilie maanani matumizi sahihi ya Kiswahili. Hili linawezekana tu iwapo mara kwa mara kutaandaliwa mafunzo maalumu yatakayowalenga wanasiasa, hususani viongozi wakuu serikalini. Ni kupitia juhudi hizi, ambapo matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi yatapewa nguvu mpya katika jamii ya Wakenya. Itakuwa rahisi kuitumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi iwapo wanasiasa watadhihirisha jitihada zao katika kuboresha matumizi ya lugha husika katika shughuli zao za kila siku. Hatua kama hii itawachochea Wakenya kujifunza lugha hii na hata kuweza kuitumia inavyowapasa katika mawasiliano.

Makala haya yameshughulikia majukumu mbalimbali yanayotarajiwa kutekelezwa na Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya. Majukumu haya ni pamoja na kutumiwa kama lugha ya kufundishia masomo mengine shuleni, kutumiwa katika mfumo wa sheria, uendelezaji wa biashara kati ya Kenya na nchi nyingine; kuendeleza shughuli za serikali na kuendeleza teknolojia. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili inatekeleza majukumu haya kwa mara ya kwanza nchini Kenya, kuna uwezekano kuwa hatua hii itakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni kama vile: kuzoeleka kwa Kiingereza kama lugha rasmi, kutosambazwa kwa istilahi za Kiswahili hususan

za kiteknolojia, mitazamo hasi ya baadhi ya Wakenya kuhusu matumizi ya Kiswahili na ukosefu wa miundombinu thabiti ya kuendeleza Kiswahili. Ili kukabiliana na changamoto hizi mikakati mbalimbali yaweza kuzingatiwa kama vile kuundwa kwa baraza maalumu la kushirikisha shughuli za kuendeleza matumizi ya Kiswahili; serikali kutenga rasilimali kwa ajili ya kueneza matumizi ya Kiswahili, matumizi ya vyombo vya habari katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili, na viongozi wa kisiasa kutambua umuhimu wa kutumia Kiswahili, sahihi katika mawasiliano yao katika miktadha mbalimbali.

## Marejeo

Bunyi, G.W (1999), Rethinking the place of African Indigenous Languages in African Education. *International Journal of Education Development, 19,* 337-350

Fasold, R (1984), *The Sociolinguistics of Society*. Oxford: Basil Blackwell

John, R.E (1998). *Language in Canada*. Cambridge: Cambridge University Press. Retrieved on May 3, 2011 from http://en.m.wikipedia.org/wiki/chart

Kachru, Braj B (1986a), *The Alchemy of English. The Spread, Functions & Models of Non-Native Englishes*. Oxford: Pergamon Press Ltd

Kimemia, J.N (2001), *Kiswahili: The Dilemma of Developing the National Language*. Njoro: Egerton University Press

Mbaabu, I (1996), *Language policy in East Africa*. Nairobi: Educational Research and Publication

Momanyi, C (2009), The Effects of 'Sheng' in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools. *The Journal of Pan African Studies, Vol. 2. no. 8, March 2009*

Olumola, S (2011), *Prof. Shitemi: Let us Commoditize and Franchise Kiswahili Language*. Retrieved on April 24, 2011 from http://www.muk.ac.ke

Patel, N (2000), *Competing Visions of Equality & Identity: Quebec's Bill 101 and Federal Language Policy*. University of British Columbia, M.A Thesis (Published). Retrieved on May 22, 2011 from circle.ubc.ca/bitstream/handle/...

Platt, J Weber, H na Ho, H.L (1984), *The New Englishes*. London: Routledge & Kegan Paul

Republic of Kenya (1964), *Kenya Education Commission Report Part 1 (Ominde Report)*. Nairobi: Government Printer

Richard, Y.B (1984), *Conflict & Language Planning in Quebec*. Clevedon, Avon, England: Multilingual Matters. Retrieved on May 3, 2011 from http://en.m.wikipedia.org/ wiki/chart...

Tully, M (1997), English: An Advantage to India? In *ELT Journal Vol 51 no. 2: 157 – 164.*